

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE**

01

KISWAHILI

Muda Saa 1:30

Mwaka: 2018

Maelekezo

1. Mtihani huu una sehemu A, B, C, D na E zenye jumla ya maswali **matano (5)**.
2. Jibu maswali **yote** katika kila sehemu.
3. Sehemu A, B, C, D na E zina alama **kumi (10)** kila moja.

SEHEMU A: (Alama 10)

1. Sikiliza kwa makini sentensi zinazosomwa kisha uziandike kwa usahihi katika nafasi zilizoachwa wazi.
 - (i) _____
 - (ii) _____
 - (iii) _____
 - (iv) _____
 - (v) _____

SEHEMU B (Alama 10)

2. Andika umoja na wingi wa sentensi zifuatazo; kipengele cha (i) kimetumika kama mfano.
 - (i) Umoja: Kiti chake kimevunjika.
Wingi: Viti vyake vimevunjika.
 - (ii) Umoja: Hiki ni kitabu changu.
Wingi: _____
 - (iii) Umoja: Kiatu changu cheupe kimepotea.
Wingi: _____
 - (iv) Umoja: _____
Wingi: Wapishi wamepika chakula kitamu.
 - (v) Umoja: Kalamu yako ilipotea darasani.
Wingi: _____
 - (vi) Umoja: _____
Wingi: Miti hii ilianguka juzi.

SEHEMU C (Alama 10)

3. (a) Kamilisha methali ulizopewa kwa kuandika jibu sahihikatika nafasi zilizoachwa wazi.
 - (i) Fahali wawili _____
 - (ii) Mvumilivu, _____

- (b) Toa maana ya methali zifuatazo kwa kuandika jibu sahihi katika nafasi zilizoachwa wazi:
 (i) Kidole kimoja hakivunji chawa _____
 (ii) Ahadi ni deni _____
- (c) Nahau “tia doa” ina maana gani? _____

SEHEMU D (Alama 10)

4. Weka alama za uandishi katika sentensi zifuatazo kwa **kuandika alama sahihi** katika nafasi iliyoachwa wazi.
- (i) Je _____ utafika saa ngapi _____
 (ii) Embe _____ nanasi na papai ni matunda _____
 (iii) Loo _____ kwani wewe ni nani _____
 (iv) Oyee _____ nani amefunga goli _____
 (v) Haba na haba _____ hujaza kibaba _____

SEHEMU E (Alama 10)

5. Soma kwa makini shairi lifuatalo kisha jibu maswali yanayofuata kwa kuandika jibu lililo sahihi katika nafasi iliyoachwa wazi.

Nchi yangu naipenda, hakika nawaeleza,
 Ni nchi yenye matunda, huwezi kuyamaliza,
 Na asali tunapenda, nchi yajitokeza,
 Tanzania Tanzania, nchi yangu nakupenda.

Kuna mrefu mlima, Kilimanjaro twakwea,
 Ardhi ya wakulima, rutuba imeenea,
 Pia mbuga za wanyama, Mikumi nawaambia,
 Tanzania Tanzania, nchi yangu nakupenda.

Tamati ninaishia, mengi nimewaeleza,
 Kabla sijaishia, mito ninawaeleza,
 Bahari pia sikia, na maziwa yapendeza,
 Tanzania Tanzania, nchi yangu nakupenda.

Maswali:

- a) Nini maana ya neno “tamati” kama lilivyotumika katika ubeti watatu?

- b) Shairi hili linahusu nini? _____
- c) Taja mlima mrefu uliotajwa na mshairi. _____
- d) Taja mbuga ya wanyama iliyotajwa katika shairi. _____
- e) Taja vyanzo viwili vya maji vilivyotajwa katika shairi hili. _____